

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU



Dodoma
10 Aprili, 2026

Barua pepe: press@ikulu.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

RAIS SAMIA AZINDUA MINARA 758 YA MAWASILIANO, AAGIZA HUDUMA ZIWAFIKIE WANANCHI WOTE

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, leo amezindua minara 758 ya mawasiliano, maunganisho ya Mkongo wa Taifa katika wilaya 85 nchini, na kushuhudia makabidhiano ya miundombinu ya mawasiliano kwa Serikali, katika hafla iliyofanyika kwenye Kituo cha Mikutano cha Jakaya Kikwete, mkoani Dodoma.

Rais Dkt. Samia amesema uwekezaji huo unaimarisha uchumi wa kidigitali na kupanua huduma za mawasiliano, hususan vijijini na mipakani, akibainisha kuwa mawasiliano sasa ni nguzo muhimu ya uchumi, uwekezaji na utoaji wa huduma za kijamii.

“Dunia ya sasa inabadilika kwa kasi. Mawasiliano si tena huduma ya anasa bali ni nguzo ya uchumi wa kisasa,” amesema Rais Dkt. Samia na kuongeza kuwa uwekezaji huu utafungua fursa za ajira, biashara na ubunifu kwa wananchi.

Aidha, Rais Dkt. Samia ameiagiza Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kuhakikisha wilaya ambazo bado hazijafikiwa na mkongo wa taifa zinaunganishwa kwa wakati, na baada ya hapo juhudi zielekezwe katika ngazi za chini zaidi ili wananchi wengi zaidi wanufaike na fursa za uchumi wa kidijitali.

Sambamba na hilo, amezitaka halmashauri zote nchini kuondoa urasimu katika utoaji wa vibali vya miradi ya mawasiliano ili kuharakisha utekezaji wa miradi hiyo kwa wakati, akibainisha kuwa ucheleweshaji wa vibali huongeza gharama za uwekezaji na kuchelewesha huduma kwa wananchi.

Vilevile, Rais Dkt. Samia amesisitiza ulinzi wa miundombinu ya mawasiliano, akiitaja kuwa ni rasilimali ya kimkakati kwa uchumi na usalama wa taifa, pamoja na kuagiza usimamizi wa huduma za mawasiliano zinazotolewa nchini kuzingatia maadili, mila na utamaduni wa Mtanzania.



Rais Dkt. Samia pia amesisitiza uwekezaji katika ubunifu wa kidijitali na kuwawezesha vijana, akibainisha kuwa hatua hiyo itaongeza ajira na ushindani wa kimataifa.

Kwa upande wake, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Angellah Kairuki, amesema mafanikio hayo ni matokeo ya ushirikiano baina ya Serikali, sekta binafsi na wadau wa maendeleo, na kuongeza kuwa Serikali itaendelea kupanua miundombinu ya mawasiliano, kukuza ubunifu wa kidijitali na kuziwezesha kampuni changa za teknolojia ili kuhakikisha sekta hiyo inachangia zaidi katika ukuaji wa uchumi na utoaji wa huduma kwa wananchi.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), CPA Moremi Marwa, amebainisha kuwa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano umefika wilaya 121 kati ya 139 za Tanzania Bara, hatua inayoongeza uthabiti wa mawasiliano ya ndani na kimataifa.

Akizungumza kwa niaba ya watoa huduma, Afisa Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Yas Tanzania, Pierre Canton-Bacara, amesema sekta binafsi itaendelea kushirikiana na Serikali kuendeleza uwekezaji katika miundombinu ya mawasiliano, huku akisisitiza umuhimu wa mapitio ya gharama za miundombinu ili kuongeza ushindani wa kikanda na kuvutia matumizi ya data.

Pembeazoni mwa uzinduzi huo, Rais Dkt. Samia pia ameshuhudia utiaji saini wa makabidhiano ya miundombinu ya Mkongo wa Taifa Serikalini, na kugawa tuzo kwa kampuni za mawasiliano zilizoshiriki katika utekelezaji wa miradi hiyo.



Shaaban Kissu

K.n.y. Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu